Nilikuwa na bahati kuwa mgeni rasmi hapahapa mwaka wa elfu mbili na saba. Kwa hiyo ninyi mnaohudhuria shule mara ya mwisho leo, labda umeshanisikiliza. Basi, nakuombeni kunisikiliza tena!

Huu ni wakati maluum kwa wanafunzi wa darasa la saba. Kusoma shule ya msingi kumekwisha. Sasa mnaweza kufikiri kuhusu likizo ndefu tu, lakini leo ningependa nyinyi kufikiria sana kuhusu mambo matatu.

Nataka kila mmoja kuangalia nyuma na kupima kwamba umetumia ile miaka saba vizuri. Je, umepata marifiki? Je, umesoma vizuri na umejifunza umuhimu wa kazi? Na Je, umejenga uweza wa kufikiri?

Mambo matatu ni: marafiki; kazi na uwezo wa kufikiri.

**Marafiki:** Kili mmoja duniani anahitaji rafiki. Naongea kuhusu rafiki – na sio mpenzi. Kila mmoja anapaswa kuhakikisha asikae peke yake. Maishi ni magumu na marafiki ni muhimu. Wasichana wana uwezo kupata na kubaki na marafiki zaidi ya wavulana. Kupata rafiki wewe mwenyewe unapaswa kuwa rafiki. Maana ni kukaa kirafiki, kusaidia, kutetea, pamoja na kufurahisha. Ukitoa utapata. Rafiki mzuri ni mtu atakayeweza kukaa nawe na kutoa mawazo, na kutoa ushauri wa kukusaidia. Pia atakayeshirikiana nawe (labda vitu kama vitabu, nguo au chakula, au jambo kama muda wake, furaha yake pamoja na huzuni yake). Kwa upande wa wavulana nakushauri kutokusahau kujenga marafiki. Kuna wanaume wengi ambao hawana rafiki mzuri kuweza kukaa naye na kupata msaada, ushauri au furaha.

Lakini muhimu mno ni kuchagua rafiki na busara. Ukianza urafiki na mmoja anayevuta bangi, nafasi ya wewe kupotea njia ni kubwa. Rafiki akicheza darasani bila kusoma itawezekana atakushawishi kucheza pia. Kamwe usiogope kuacha rafiki ukiona atakupelekea hali mbaya.

**Kazi:** Sasa mnaweza kufikiri kwamba likizo ndefu bila kuja shuleni ni nzuri. Sawa, lakini hii likizo ikiendelea kwa miezi baada ya miezi utasikiaje? Kila mtu anahitaji kazi za kufanya. Kila mtu anataka kufaa. Kila mtu ana nafasi yake ndani ya jamii, na kila mtu anastahili kuweza kusema anachofanya. Je, unafanya nini cha kufaa? Unafanya nini kusaidia? Unafanya nini kuwa sehemu ya jamii?

Je, unasaidia kukatia ng'ombe? Unachukua maji? Unalima? Unafua nguo? Unaimba kwaya? Unatembelea bibi na babu kuongea nao? Unasaidia wadogo zako? Je, unaamka kitandani kufanya nini? Kama hujui – basi una muda sasa kujitazama na kuanza kupanga. Kukaa bila kazi ni kosa kubwa – ni dhambi kweli – na hutafurahi.

Baadhi yenu mtakwenda kusoma sekondari. Lakini usiwe haraka kuringa. Siku hizi hali ya elimu sio juu, na wengi wengi wanamaliza kidato cha nne na Division Four. Hii ni kama sifuri – na ni maana umepoteza pesa za wazazi na muda wako. Ukipata nafasi kusoma sekondari ni juu yako kutumia fursa ile, kusoma kwa bidii. Narudia – chagua marifiki kwa makini na busara ili usome badala ya kucheza na kupotea nafasi.

Baadhi yenu hatutaenda sekondari. Je, mtafanya nini? Labda utasikia kama umeshindwa. Sawa – kushindwa ni kujifunza. Mimi mwenyewe nilishindwa mitihani ya muhimu mno Uingereza. Sikufaulu vizuri kidato cha sita na A levels. Lakini kutokufaulu kulinipa somo

zuri kuliko yote. Niligundua maana ya kazi. Nilikuwa nimecheza kidogo badala ya kusoma. Nilanza na nia ya kufaulu na kukazana. Na mpaka leo nafahamu – nikitaka kupata kitu ni juu yangu kufanya kazi nakukipata.

Lakini – kuamua unataka nini? Hii inategemea uwezo wako kufikiri.

**Kufikiri:** hili ni jambo la tatu, na ni muhimu kuliko yote. Kama unao uwezo kufikiri vizuri basi utaendelea vizuri na maisha yako. Kufikiri – maana yake ni kusimama na kufikiri kuhusu mambo na kutokukimbia kufanya uamuzi. Ya kwanza ni uamuzi kuhusu unachotaka kufanya. Ya pili ni uamuzi kuhusu namna ya kuifanya. Kabla ya kuamua, inabidi ukae chini na kupima uchaguzi.

Kama hupati nafasi sekondari – je, utafanya nini – na utapenda kufanya nini? Namna na kuchagua na kuamua?

Nimeishi hapa nchini kwa miaki mingi sasa na nimeona mabadiliko. Zamani baada ya kusoma shule ya msingi kila msichana alitaka kusoma ushonaji (hata kama hakuna kazi baada ya kusoma) na kila mvulana alitaka kusoma useremala. Sasa – ni ‘fashion’ au ‘kileo’ kwenda sekondari hata kama mwanfunzi hana uwezo kukaa dawatini na kusoma.

Usivutwe na mambo ya kileo (au fashion). Kaa kufikiri kuhusu uwezo wako, shauku yako na lengo lako.

Je, kweli una akili ambayo inafaa kusoma ya kielimu? Sio kila mtu kufaa kusoma hivyo.

Labda una akili ambayo inafaa kabisa ya kifundi (pamoja na kilimo). Kaa kufikiri na kupima ni nini inakuvutia?

Pia nakushauri kutokufikiria pesa. Wengi wanasema wanataka kuwa wakili – kwa sababu wanataka pesa –na sio kwa sababu wanavutiwa na kazi za wakili. Hii sio kufikiri na busara. Fikiri tu kuhusu kitu ambacho unataka kukifanya na sio kuhusu unachotaka kupata. Ukipenda kazi, utafanya kwa bidii na utapata mafanikio.

Ukipata nia kuna njia. Baada ya kuamua unataka kufanya nini, halafu anza na kufikiri namna ya kuipata. Mtu akiwa na lengo peke na anaonyesha nyia kabisa mimi sidhani atakosa msaada.

Pia maisha yangu sijaona ujuzi na uwezo kupitiwa na vyeti. Nina maana – pata ujuzi na uwezo juu, na usijali sana na kupata cheti. Cheti peke yake sio kitu. Ukipata ujuzi unaweza kupata cheti kwa rahisi baadaye.

Pamoja na kufurahia ya kumalizi hii hatua ya maisha yenu, nakuombeni pia kuchukua dakika chache baadaye kudhani kuhusu hayo mambo matatu: Marafiki; Kazi na Uwezo wa kufikiri.

Nakutakieni kila la heri.